JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO, VYUO VYA UALIMU NA VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI MWAKA, 2020

Imeandaliwa na:

Idara ya Usimamizi wa Elimu
Seksheni ya Sekondari
Barua pepe: dea@tamisemi.go.tz

Juni, 2020

1.0 UTANGULIZI

Zoezi la uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule za Sekondari za Serikali, Vyuo vya Ualimu, na Vyuo vya Elimu ya Ufundi kwa mwaka 2020, limefanyika na kukamilika. Zoezi hili limefanyika kwa kuzingatia takwimu za matokeo ya watahiniwa waliofanya Mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2019 kutoka Tanzania Bara, idadi ya nafasi za Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya Elimu ya Ufundi pamoja na Vigezo vya Uchaguzi wa Wanafunzi vilivyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

1.1. TAKWIMU ZA WATAHINIWA WA MTIHANI WA KIDATO CHA NNE, 2019

Watahiniwa wa shule **425,072** wakiwemo wasichana **221,813** na wavulana **203,259** walifanya mtihani wa kuhitimu Kidato cha Nne mwaka, 2019. Aidha, Watahiniwa wa Kujitegemea **48,683** walifanya Mtihani huo mwaka, 2019.

Jumla ya wanafunzi **121,251** wakiwemo wasichana **53,829** na wavulana **67,422** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano, Vyuo vya Ualimu, na Vyuo vya Elimu ya Ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Idadi hii ni sawa na asilimia **93.4** ya wanafunzi wenye sifa za kuchaguliwa.

2. UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO, VYUO VYA UALIMU NA VYUO VYA ELIMU YA UFUNDI,

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka **2020** ni wale waliotoka Shule za Serikali, zisizo za Serikali, waliosoma nje ya mfumo rasmi na waliosoma nje ya nchi baada ya matokeo yao kupata

ulinganifu wa Baraza la Mtihani Tanzania. Jumla ya shule za sekondari **434** zikiwemo shule **32** mpya za Kidato cha Tano zilizoanza mwaka huu zimepangiwa wanafunzi.

2.1 WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA MASOMO YA KIDATO CHA TANO

Jumla ya wanafunzi **73,101** wakiwemo wasichana **35,005** sawa na asilimia **47.9** na wavulana **38,096** sawa na asilimia **52.1** wamechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano.

Kati ya wanafunzi **73,101** waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano;

i) Wanafunzi **36,365** wakiwemo wasichana **15,631** na wavulana **20,734** wamechaguliwa kusoma masomo ya Tahasusi za Sayansi na Hisabati;

ii) Wanafunzi **36,736** wakiwemo wasichana **19,374** na wavulana **17,362** wamechaguliwa kusoma Tahasusi za masomo ya Sanaa na Biashara;

iii) Miongoni mwa wanafunzi waliochaguliwa, jumla ya wanafunzi **1,572** wakiwemo wasichana **685** na wavulana **887** wamechaguliwa kujiunga na Shule za wanafunzi wenye Ufaulu Mzuri Zaidi (Vipaji Maalum), wakiwemo wanafunzi **4** wavulana wenye Mahitaji Maalum.

iv) Miongoni mwa waliochaguliwa, wanafunzi **183** ni wenye **Mahitaji Maalum** (wasichana **82** na wavulana **101).**

v) Aidha, jumla ya wanafunzi **154** wakiwemo wasichana **59** na wavulana **95** waliosoma Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kupitia na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima wamechaguliwa pia kujiunga na masomo ya Kidato cha Tano.

2.2 WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA VYUO VYA YA UFUNDI, VYUO VYA AFYA NA VYUO VYA UALIMU

Jumla ya wanafunzi **9,264** wakiwemo wasichana **4,314** na wavulana **4,950** wamechaguliwa kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Ufundi, Vyuo vya Afya na Vyuo vya Ualimu kwa mchanganuo ufuatao;

JEDWALI 1: IDADI YA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA STASHAHADA YA KADA MBALIMBALI

Na	Maelezo	Wasichana	Wavulana	Jumla
1	Vyuo Vinne vya Ufundi(Stashahada)	621	985	1,606
2	Vyuo vya Afya(Stashahada)	1004	883	1887
3	Stashahada ya Ualimu (Sayansi)	525	825	1,350
4	Stashahada ya Ualimu (Elimu ya Msingi)	2,164	2,257	4,421
Jumla		**4,314**	**4,950**	**9,264**

2.3 WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA KUJIUNGA NA VYUO VYA KADA MBALIMBALI

Jumla ya wanafunzi **38,886** wakiwemo wasichana **14,510** na wavulana **24,376** wamechaguliwa kujiunga na Vyuo vya Elimu ya Ufundi vinavyosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Wanafunzi hao wamepangwa katika vyuo na taasisi mbalimbali kama vile Ardhi, Biashara, Maendeleo ya Jamii, Uvuvi, Mifugo, kilimo, Mazingira, Mipango ya Maendeleo Vijijini na nyinginezo. Orodha ya vyuo na idadi ya wanafunzi imeambatishwa.

3.0 MAELEKEZO KWA WANAFUNZI WALIOCHAGULIWA

3.1 Wanafunzi wa Kidato cha Tano:

Wanafunzi wote wa **bweni** waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano mwaka, 2020 wanatakiwa kuripoti shuleni tarehe **18 Julai,**

2020 tayari kwa kuanza masomo tarehe **20 Julai 2020**. Aidha, wanafunzi wa **kutwa** waripoti na kuanza masomo tarehe **20 Julai 2020.** Wanafunzi ambao hawataripoti wiki mbili tangu tarehe ya kufungua shule nafasi zao zitachukuliwa na wanafunzi wengine ambao hawakupangiwa shule katika awamu hii.

Uhamisho wa shule utaruhusiwa baada ya kukamilika kwa Muhula wa Kwanza wa masomo, na zoezi hilo litafanyika kwa kuzingatia uwepo wa nafasi kwenye Shule kwa **idhini ya Maafisa Elimu wa Mikoa husika**. Hivyo, hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya Shule kwa sasa ngazi za Mikoa Halmashauri na shule.

3.2 Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundi:

Wanafunzi waliopangwa kwenye Vyuo vya Elimu ya Ufundi vilivyopo chini ya NACTE wanatakiwa:

i. **Kuthibitisha** kukubali kujiunga na kozi zinazosimamiwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) baada ya siku saba (7) kuanzia siku ya kutangazwa kwa matokeo ya uchaguzi hadi tarehe 15 Agosti, 2020.

ii. Mwanafunzi atafanya uthibitisho kupitia kiunganishi kinachoitwa **Uthibitisho TAMISEMI** katika tovuti ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) ambayo ni ***www.nacte.go.tz*** ili kukubali kuchaguliwa kwenye kozi na vyuo walivyopangiwa.

iii. Mwanafunzi ambaye **hatathibitisha** kukubali nafasi aliyochaguliwa, **nafasi yake itachukuliwa** na wanafunzi wengine wanaoendelea kuomba katika Vyuo hivyo kwa njia ya mtandao.

iv. Wanafunzi wanaotaka kufanya mabadiliko ya kozi au chuo walikochaguliwa, wanaruhusiwa kufanya hivyo kuanzia **tarehe 01 Agosti hadi 30 Agosti, 2020** kupitia mtandao wa NACTE.

v. Vyuo ambavyo vimepangiwa wanafunzi, vitapata orodha ya waliochaguliwa kutoka NACTE kwa njia ya Mfumo (kupitia Institution Pannel) baada ya muda wa kuthibitisha na kuhama kukamilika.

vi. Maelekezo ya namna ya kuwasajili wanafunzi watakaoripoti Vyuoni kuanza masomo yatatolewa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE).

vii. Wanafunzi waliopangwa katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya hawatahusika na utaratibu wa kubadilisha wa NACTE, hivyo wanapaswa kuwasiliana na vyuo husika.

3. HITIMISHO

Nawapongeza walimu, wazazi na walezi wote kwa juhudi walizozifanya katika ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufaulu vizuri. Vilevile, nawapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu ya Ufundi. Napenda kutumia fursa hii, kuwahimiza kuendelea kufanya bidii katika kujifunza ili waweze kufanikiwa kujiunga na mafunzo ya elimu ya juu baada ya kuhitimu Kidato cha Sita na Stashahada zenu katika Vyuo walivyopangiwa.

Nawashukuru wadau wote wa elimu kwa maana ya viongozi na watendaji wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri zote pamoja na wananchi kwa ujumla kwa kushiriki kikamilifu kuimarisha miundombinu ya shule ikiwemo madarasa, mabweni, maktaba,

maabara na majengo mengine muhimu yaliyowezesha shule **32** mpya kuanzishwa na kupokea jumla ya wanafunzi **2,571** wakiwemo wasichana **1,584** na wavulana **987** wa Kidato cha Tano kwa mara ya kwanza.

Nitumie fursa hii pia kutoa wito kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Miji, Manispaa na Majiji kuhakikisha kuwa azma ya Serikali ya kila Tarafa kuwa na shule ya Kidato cha Tano inatekelezwa ili kuwezesha wanafunzi wote wanaofaulu Mtihani wa Kidato cha Nne kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya Kidato cha Tano na Sita.

Kwa sababu hiyo, Wakurugenzi wa Halmashauri za **Kyerwa DC**, **Momba DC**, **Mtwara DC**, **Ubungo MC** na **Nanyamba TC** ambazo hazina Shule za Kidato cha Tano na Sita wahakikishe kuwa kufikia tarehe 30 Januari, 2021 Halmashauri zao zina **Shule zenye Kidato cha Tano hususan za masomo ya Sayansi na Hisabati na ziwe zimetengewa bajeti ya chakula**.

Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Elimu ya Ufundi kwa mwaka 2020 na maelekezo ya kujiunga (Joining Instructions) inapatikana kwenye tovuti ya OR-TAMISEMI ya **www.tamisemi.go.tz**

Ahsanteni kwa kunisikiliza.

Selemani S. Jaffo (**Mb**)

WAZIRI WA NCHI, OR-TAMISEMI